# Habari za Jimbo la Tanga

*Kama zilivyoandikwa na Afisa wa Habari kwa idhini ya Regional Comissioner, Tanga*

**No. 32** **Gazeti hili hutolewa bure.** **Septemba, 1963**



**Rais wa Tanganyika Mwalimu Julius Nyerere anashuka katika gari la moshi alilokuja nalo ili kufungua reli mpya ya Ruvu-Mnyuzi. Hapa ni stesheni ya Makinyumbi.**

## RAIS AFUNGUA NJIA YA RELI

Tarehe 17 Agosti, Rais wa Tanganyika, Mwalimu Julius Nyerere aliifungua rasmi reli kati ya Ruvu na Mnyusi. Kufunguliwa kwa reli hii kulifanyika katika stesheni mpya ya Makinyumbi mbele ya hadhara kubwa iliyohudhuriwa na watu wa mataifa yote.

Reli hii sasa imeunganisha Afrika Mashariki nzima, kwahio bidhaa na abiria watasafiri moja kwa moja kutoka Tanga hadi Dar es Salaam, au kutoka Dar es Salaam mpaka Mombasa, Nairobi na Kampala. Kadhalika nauli imepunguzwa.

Katika hutuba ya kuifungua reli hii mpya iliyogharimia pauni milioni tatu, Rais alisema kwamba ubora na umuhimu wa reli hii unaonekana wazi, na utaendelea kuwa hivyo kwa miaka mingi ijayo.

Njia bora za kupeleka bidhaa na watu ni za maana sana kwa kazi ya kujenga Taifa na maendeleo ya nchi, na reli hii imefanya kupatikana kwa jimbo hili, pamoja na kuziunganisha nchi hizi za Afrika Mashariki pamoja.

### RELI YA TANGA

Reli ya Tanga sasa ni 70 tangu kutengenezwa na ni reli ya kwanza nchini. Ilianzishwa mwaka 1893 na Wajerumani.

Watu wote walioajiriwa katika Idara ya Reli wanafanya kazi ya thamani kubwa kwa Tanganyika kwa kuwashinda maadui wakubwa — umaskini, magonjwa na ujinga, na ni lazima wawe wenye fahari kwa kazi zao kwa manufaa ya nchi. Kwa vile bila ya reli mazao katika vijiji yangeharibiwa na yasingefika yanakotakiwa. Wagonjwa wasingeweza kufika katika Hospitali kubwa na watoto wa Skuli wasingeweza kusafiri kwenda kwenye vyuo vyao.

## SERIKALI YAHESHIMU DINI

Serikali ya Tanganyika inaheshimu uhuru na kazi za dini zote. Uhuru wenyewe ukiwa wa kuabudu, mikutano ya dini na kuieneza dini. Maneno haya alisema Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Bwana Job Lusinde.

Pia serikali inatoa ruhusa katika sikukuu za dini, pia wafanya kazi wanapewa ruhusa siku za kazi kwenda kusali na kushiriki katika sherehe nyingine za dini.

Lakini ikiwa kiongozi yeyote wa dini atatumia dini kama ngao ya kueneza siasa yake au ya mtu mwingine, na kama kiongozi yeyote wa dini anaitumia dini kuleta farakano kwa nchi hii, basi Serikali haitasita kumchukulia hatua kali.

## 13 Wasio na kazi wahamishwa Tanga

Watu 13 wasio na kazi na ambao walionekana wanazurura ovyo mjini, walirudishwa makwao na Area Kamishna wa Tanga, Bwana Ali Diwani.

Katika kundi hilo watu wengine walipelekwa Mwanza, Bukoba, Arusha, Dodoma, Lushoto na Handeni, na walisafirishwa kwa nauli ya Serikali.

Mapema mwezi jana, Bwana Diwani aliwaonya watu wasio na kazi wajitafutie kazi za kufanya, au warudi makwao wakalime, alisema kama hawafanyi hivi Serikali itachukua hatua.

Bwana Diwani aliwaambia watu kwamba wasio na kazi katika mji wanaweza kwenda kuishi Pongwe katika shamba lililofunguliwa na Serikali, ambako watapewa ardhi ya kulima, na pia chakula hutolewa bure na Serikali.

# SERIKALI YAKOPESHA FEDHA KUONDOA NYUMBA ZA MAKUTI

Kwa muda mfupi tuu wa miaka miwili na nusu Serikali Kuu na Halmashauri ya Mji wa Tanga imekopesha Shs. 560,000/— kwa watu 280 ili waezeke nyumba zao kwa mabati. Jambo ambalo halikutokea katika miaka 40 ya Serikali ya Kikoloni.

Shauri lilikatwa na Serikali ya Wananchi walipoona kuwa nyumba za makuti ni hatari sana kwa moto, na ni nia ya Serikali kufanya kila njia kuwawezesha watu wote nchini kuwa na nyumba bora na kuepuka khofu ya kuogopa moto, na hii kama inavyojulikana inahitaji mapesa mengi, na itachukuwa muda kabla watu wote nchini wamepata nyumba za mabati.

Inataka ufikirie kidogo kuona kwa watu 280 fedha iliyotumiwa ni kama hiyo hapo juu. Jee Tanganyika nzima yenye Wilaya nyingi na watu milioni kumi, itataka fedha kiasi gani kufanya kazi hii?

Ulipoingia moto mkubwa hapa Tanga, Serikali Kuu peke yake ilikopesha Shs. 300,000/— kwa watu 150 waliyounguliwa, na fedha hizi zilitolewa bila ya faida yoyote. Muda wa kulipwa ni miaka mitano. Ukifanya hisabu kufuata muda huu, utaona kiasi kidogo tu cha kiasi ya Shs. 34/— kitatakiwa kulipwa kila mwezi.

Watu wengine 50 wenye nyumba walikopeshwa Shs. 100,000/— kwa kutia mapaa ya mabati. Katika fedha hizi Serikali Kuu ilitoa Shs. 60,000/—, na Halimashauri ya Mji wa Tanga ilitoa Shs. 40,000/—. Faida kwa mkopo huu ni sehemu sita kwa mia. Wale waliyochukua Shs. 2,000/— walitakiwa kulipa kila mwezi Shs. 39/50, na wale waliokopa Shs. 1,800/— walipe Shs. 36/— kwa mwezi.

Hivi karibuni tu wananchi 80 walipewa mkopo wa kuwawezesha kutia bati nyumba zao, na Serikali Kuu safari hii ilitoa Shs. 60,000/— na Halimashauri ya Mji Shs. 100,000/— jumla 160,000/—. Kulipa ni kwa muda wa miaka 5, toka Shs. 36/— mpaka 39/50 kwa mwezi.

Sasa tujiulize sisi tuliyokopeshwa fedha hizi. Jee sisi tuu basi tumepata mapaa ya bati, jee ndugu zetu wengine wapate mkopo namna hii au wasipate?

Mwananchi bora na aliye na hamu ya kuona maendeleo ya nchi yake lazima atajibu kuwa wananchi wengine wawe na nafasi kupata mikopo namna hii. Basi kama ni hivyo, tufanyeje ili kazi hii iwe rahisi? Njia ni moja na fupi. Ni kwetu sisi tuliyopata mikopo hii kufanya kila njia ili tulipe deni letu kila mwezi. Kwa kufanya hivyo, utaona kwa muda mfupi, ndugu zetu wananchi wengine watakuwa na nafasi ya kupata mkopo katika fedha hizi hizi zetu tunazolipa.

Kama ukichukuwa watu 280 waliopata mikopo na kila mmoja akilipa Shs. 35/— (wastani), utaona kama kila mwezi zingelirudishwa katika mfuko wa kukopesha watu Shs. 9,800/—, na kwa muda wa miezi sita tuu zingalipatikana tena Shs. 588,000/— ambazo zingeliweza kukopeshwa watu kiasi ya 160 hivi. Basi kwa nini wananchi hatufanyi haya. Wengine najuwa wanalipa mikopo yao vema, lakini nasema wote wawe na moyo wa kiungwana, na kuwa na hamu ya kuwasaidia ndugu zao wengine waweze kuwa na nyumba kama zao. Haya shime wananchi tuijenge nchi yetu na hakuna njia ingine ya kuijenga nchi hii ila kila mmoja amuonee huruma mwenzake, na aone vitu vizuri alivyopata yeye apate yule asiyekuwa navyo.

# MIPANGO ZAIDI YA KUFUGIA NG'OMBE

Wananchi wa Wilaya ya Tanga, wanazidi kufungua mipango ya minazi na ng'ombe. Hivi karibuni Mheshimiwa Waziri mdogo katika Wizara ya Kilimo Bwana Barongo alifungua mpango mmoja katika kijiji cha Maranzara, sehemu ya Pongwe. Pia Mheshimiwa Bwana Rashidi Jumanne Abdallah, Mkuu wa Mkoa wa Tanga alifungua mpango kama huo katika kijiji cha Mleni. Miji yote hiyo ikiwa katika Wilaya ya Tanga.

Wananchi wa Maranzara waliweza kulima eka 800 za shamba ndani yake mkiwa na minazi 6,000 na kundi la ng'ombe wapatao 112 ambao hulishwa katika shamba hilo.

Kadhalika wananchi hao waliweza kuchanga kiasi cha Shs. 2,000/— kutengeneza nyumba ya kuwahifadhia ng'ombe wao.

Serikali ilitoa msaada, wa simenti, mabomba, waya na mashine ya kutilia dawa wanyama hao.

Vile vile wananchi hao wanatazamia kufungua shamba la katani ambalo watalilima kwa kushirikiana.

Bwana Barongo alipofungua mpango huo alisema ni nia ya Serikali kueneza mipango ya minazi na ng'ombe katika sehemu yote ya pwani. Pia aliwaomba wananchi hao washirikiane na wataalamu wa serikali kwa kuendeleza mipango hiyo.

Kule Mleni nako, Bwana Abdallah, Mkuu wa Mkoa wa Tanga alipofungua shamba hilo aliwaambia wananchi kuwa hakukuwa na mtu ambaye amezaliwa na utajiri, ila mtu yeyote ambaye ni taajiri ni lazima alifanya kazi kwa bidii kuupata utajiri huu. Na hapo aliwahakikishia kuwa iwapo watu wa Tanganyika wangefanya kazi kwa bidii, kungekuwa na mafanikio kwa nchi hii.

Jamaa hao wa Mleni ni 47, wakiwa na shamba lenye eka 412 lenye minazi zaidi ya 10,000 na kundi la ng'ombe wapatao 61. Hivi sasa mipango hiyo inaendelea vema.

# KAZI YA KUJENGA TAIFA YASONGA MBELE — PANGANI.



**Watatu kutoka kushoto ni Waziri wa Vyama vya Ushirika na Maendeleo, Mheshimiwa Bwana Kasambala, pamoja na Bwana R. J. Abdallah (katikati) mkuu wa Mkoa wa Tanga, wakishiriki kuchukuwa mawe ya kujengea cliniki huko Pangani, inayojengwa na wananchi wenyewe.**

# TWENDENI TUKASOME

Kama wewe unajua kulisoma gazeti hili, basi tunakuita una bahati. Wako ndugu zetu wengi sana ambao hawajui kusoma wala kuandika, basi Serikali ya wananchi ikaona ni wajibu wake mkubwa kuanzisha madarasa ya watu wazima ili wafundishwe kusoma na kuandika.

Tokea yaanze madarasa haya, wake kwa waume wamehudhurua na kujifunza, na sasa wanaweza kusoma magazeti na kuandika barua kwa jamaa zao.

Watu wengi wamejitolea kufundisha katika madarasa haya, na kusa'dia kwao kumeleta faida kubwa nchini. Lakini bidii yote ni juu ya watu wenyewe wasiojua kusoma wala kuandika kuandikisha majina yao katika madarasa haya kwa faida yao.

Serikali imeanza kuonyesha njia, na iko tayari siku zote kuona kuwa wananchi wanajua kusoma na kuandika, na kila bidii inafanywa na Idara ya Maendeleo pamoja na ushirika na Idara nyingine za Serikali kuhakikisha kuwa jambo hili linafanikishwa, lakini kufanikishwa kwake ni lazima wananchi wenyewe waonyeshe moyo wa kuhudhuria katika madarasa haya.

Katika mkoa huu wa Tanga madarasa mengi yamefunguliwa, katika Wilaya zote, na wananchi wanaonyesha bidii sana na wana moyo wa kuendeleza elimu yao, basi tunawataka wananchi wengine katika kila sehemu Jimboni wajiandikishe katika madarasa haya.

Labda utauliza jee, mimi ni mzee nitachukuwa muda mrefu hata kusoma na kuandika kwa muda mfupi tu. Basi hakuna sababu na wewe usijiunge katika madarasa ya watu wazima sasa. Hakuna wakati wa kupoteza, huu ni wakati mzuri, ambao kama hutautumia vema kwa manufaa yako, kwa manufaa ya nchi yako na jamaa yako, basi utakuja kujuta.

Umuhimu wa kusoma umekwishajulikana wazi kote nchini, na watu wengi sasa wanajisaidia wenyewe, na pia wamegundua kama hakuna taklifu yoyote kujifundisha kusoma. Pia tunajua wale waliopata bahati ya kujua kusoma na kuandika kila mara wako tayari kusaidia ndugu zao waweze kumuondoa adui ujinga.

## TAREHE ZA USHURU ZAONGEZWA

Waziri wa Serikali za Mitaa, Bwana Austin Shaba ametoa uamuzi wake kuhusu mageuzo katika tarehe ya mwisho ya kulipa ushuru (local rates) bila nyongeza ya adhabu.

Amesema kwamba badala ya tarehe 31/8/63 sasa itakuwa 31/10/63 ndipo ushuru wote uwe umelipwa.

Basi ni juu ya wananchi wote wanaohusika, wafanye bidii kulipa ushuru wao kabla ya tarehe hiyo mpya kumalizika, yaani 31/10/63.

Printed by the Vuga Press, Soni Tanganyika